**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

Namba za Simu

**Mkuu wa Shule 0782773388**

**Makamu Mkuu wa Shule 0768112082**

**Matron 0787296781 /0652972324**

**Shule ya Sekondari MVUMI MISSION**

**S.L.P 78- MVUMI DODOMA**

**Tarehe ..................................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**
**.................................................**
**S.L.P ..........................................**
**.................................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MVUMI MISSION HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO MKOA WA DODOMA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya HGK

Shule ya Sekondari **MVUMI MISSION** ipo umbali wa Kilometa 40 Kusini Mashariki mwa Mji wa Dodoma.
kutoka stendi kuu Dodoma (Nanenane) utapanda daladala hadi kituo daladala mjini (sabasaba) nauli ni Tsh 500/= ukishafika stendi ya daladala sabasaba utachukua bodaboda( pikipiki) kwenda stendi ya majengo kilipo kituo cha daladala za kuja Mvumi mission na nauli ni tshs 1500/= kituo kinapatikana maeneo ya majengo karibu na soko la majengo. Usafiri wa daladala kutoka majengo hadi mvumi mission ni shs. 4000/= na kutoka stendi ya mvumi mission mpaka shule ilipo unapanda bodaboda(pikipiki) kwa tshs 1000/=
N.B. utokapo mjini kuja mvumi mission tafadhari usishuke kituo chochote cha njiani kituo ch mwisho ndo kituo ambapo magari huwa yanafika ukomo wa safari ambacho ni kituo cha mvun mission.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **13/07/2024** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shule tarehe **13/07/2024** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/07/2024**

Mambo muhimu ya kuzingatia: -

CamScanner

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili (2) ndefu za **Dark blue** kwa Wasichana urefu ifike kwenye kifundo cha mguu. Maelezo ya mshono ni **Rinda box** ( rangi ya kitambaa imeambatanishwa hapo chini)
ii. Mashati mawili (2) meupe mikono mirefu
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama kwa waisilamu ,kwa wanafunzi wa kiislamu hawaruhusiwi kushona suruali na wao pia washone sketi
iv. Sare ya Michezo ni track suit nyeusi na raba za michezo
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe
vii. Sweta moja rangi ya dark blue lenye shingo ya V .
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) aje na gauli mbili (2) ndefu za rangi ya dark blue.
ix. Tai yenye michirizi ya rangi dark blue na nyeupe
x. Tisheti (2)(T-shirt) ambazo zitapatikana shuleni

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 8 (*Quire 3*);
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa kwa chini mwanafunzi aje angalau na kitabu kimoja cha kila somo kwenye tahasasu yake*);
iv. Scientific Calculator;
v. Godoro moja (1). (saizi ya godoro ni futi 3x6)
vi. Mashuka Jozi 2 rangi ya pinki, blanket 1, chandarua 1 (*blue );*
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Jembe 1 na mpini wake , reki 1, mifagio 1 wa ndani (soft bloom ).

N.B **. kila mwanafunzi ni lazima awe na bima ya afya.**

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ili rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolew Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMIS yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mamb msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara b ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

CamScanner

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.,
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii,
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## . Viambatisho na Fomu Muhimu

CamScanner

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iii. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. *Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.*

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

..............................................

**PETER NASON MLUGU**

**MKUU WA SHULE**

THE HEADMASTER
MVUMI MISSION SEC. SCHOOL
P. O. Box 78, DODOMA
DATE:.................... SIGN.............

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na wat wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husi ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pes TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WA USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0782773388**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0768112082**
- **Mwandamizi Taaluma 0742356098**
- **Mwandamizi Malezi 0714892293**

## AINA YA VITAMBAA



dark blue

CS CamScanner

**MVUMI MISSION HIGH SCHOOL**
**MEDICAL CERTIFICATE FORM**

To be completed by Medical Officer in Government Hospital.

Full Name: ..........................................................................................
Age: ..................................................................................................

1. "AIDS" Test..............................................................................
2. Blood count (Red and White) ....................................................
3. Urine examination......................................................................
4. Stool examination......................................................................
5. Syphilis Test..............................................................................
6. T.B Test....................................................................................
7. Ear Test....................................................................................
8. Eye Test...................................................................................
9. Spleen.......................................................................................
10. Abdomen..................................................................................
11. Addition information of any other physical, mental hereditary of infectious diseases..............................................................................................................
..................................

Treatment after examination..........................................................................
.......................................................................................................................

*(Please state nature of treatment)*

MEDICAL CERTIFICATE:

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue further education.

Signature.......................................

Designation ...................................

Station.......................................

Date............................... Official Stamp...............................

CamScanner

**MVUMI MISSION HIGH SCHOOL**
**FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI**
**HABARI ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili la mzazi/mlezi.......................................................................
2. Kazi yake..................................................................................................
3. Nyumbani kwa baba (alipozaliwa mtoto)

   Kijiji/Mtaa................................ Wilaya...........................................
   Kata......................................... Mkoa.............................................
   Tarafa........................................
4. Anwani ya makazi pa kazi pa mzazi/mlezi...................................
   ........................................................................................................
5. Nambari ya simu.......................................................................................
6. Mimi.................................................................... (Baba/Mama/Mlezi wa ............................................. Nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo na kuwa nitawajibika kumhudumia gharama zote zitakazohitajika akiwa shuleni.

Jina........................................................................

Sahihi....................................................................

Tarehe....................................................................

CamScanner

## ORODHA YA VITABU KWA TAHASUSI ZA HGK.

### 1.KISWAHILI

- RIWAYA

-USIKU UTAKAPOKUCHA
-VUTA NIKUVUTE
-MFADHILI

- TAMTHILIA

-MORANI
-NGUZO MAMA

- USHAIRI

-KIMBUNGA
-CHUNGU TAMU
-FUNGATE YA UHURU

**VITABU VINGINE VYA KISWAHILI 1&2**

-NADHALIA YA KISWAHILI –D. T MSABILA

-KISWAHILI KIDATO CHA TANO –OXFORD

-KISWAHILI KIDATO CHA TANO-TAASISI YA ELIMU TANZANIA (TET)

-TAHAKIKI

### 2.HISTORY 1&2

-ESSENTIAL ADVANCED LEVEL –SALEH YASIN

-UNDERSTANDING AFRICAN HISTORY-APE NETWORK

-FUNDAMENTAL ADVANCED LEVEL-AVELIUS THOBIAS

### 3.GEOGRAPHY 1&2

-PHYSICAL GEOGRAPHY -D. T MSABILA OR ZISTI KAMILI

-HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAHY –D. T MSABILA

-PHYSICAL GEOGRAPHY ALIVE –ZISTI KAMILI

-GEOGRAPHY BUNETT.



CamScanner